

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

BUNGE LA TANZANIA



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA KUMI NA MOJA

KIKAO CHA KUMI

19 APRILI, 2023



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA KUMI NA MOJA

KIKAO CHA KUMI – TAREHE 19 APRILI, 2023

I. DUA:

II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (UTUMISHI NA UTAWALA BORA):

Hotuba ya Bajeti ya Ofisi ya Rais (Utumishi na Utawala Bora) kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024.

MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UTAWALA, KATIBA NA SHERIA:

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Ofisi ya Rais (Utumishi na Utawala Bora) kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024.

III. MASWALI:

OFISI YA WAZIRI MKUU:

123. MHESHIMIWA BONNAH LADISLAUS KAMOLI (SEGEREA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu:-

Je, ni Watanzania wangapi wamejitokeza na kupata fursa ya mafunzo maalum ya ujuzi yaliyotangazwa kupitia VETA kote nchini.

OFISI YA RAIS (TAMISEMI):

124. MHESHIMIWA DEUS CLEMENT SANGU (KWELA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, Serikali ina mpango gani wa kupanua Kituo cha Afya cha Laela na kuwa katika hadhi ya Hospitali ya Wilaya.

125. MHESHIMIWA LEAH JEREMIAH KOMANYA (MEATU):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, kuna mpango gani kukamilisha ujenzi wa maboma ya Ofisi Kata za Nkoma, Mwangudo, Mwamanimba na Imalaseko - Meatu.

OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO NA MAZINGIRA):

126. MHESHIMIWA JEREMIAH MRIMI AMSABI (SERENGETI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira):-

Je, kuna mpango gani wa kudhibiti mafuriko katika Mto Mara kwa kuvuna maji kupitia Mabwawa na kujenga Skimu za Umwagiliaji.

WIZARA YA KILIMO:

127. MHESHIMIWA GEORGE RANWELL MWENISONGOLE (MBOZI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:-

Je, ni lini Serikali itaondoa makato yaliyopo kwenye Vyama vya Msingi kwa Wakulima wa Kahawa Mbozi.

WIZARA YA UWEKEZAJI, VIWANDA NA BIASHARA:

128. MHESHIMIWA NEEMA KICHIKI LUGANGIRA (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara:-

Je, Serikali imejiandaaje kuweka mazingira wezeshi ya uwekezaji nchini.

WIZARA YA MALIASILI NA UTALII:

129. MHESHIMIWA YAHYA ALLY MHATA (NANYUMBU):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii:-

Je, ni Wananchi wangapi wa Jimbo la Nanyumbu wamefidiwa kutokana na uharibifu uliofanywa na Tembo katika mashamba yao.

WIZARA YA NISHATI:

130. MHESHIMIWA COSATO DAVID CHUMI (MAFINGA MJINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nishati:-

Je, ni lini Mafinga itanufaika na mradi wa umeme wa *Peri-Urban*.

WIZARA YA AFYA:

131. MHESHIMIWA HUSNA JUMA SEKIBOKO (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kudhibiti matumizi holela ya Dawa za Binadamu nchini.

132. MHESHIMIWA ASIA ABDUKARIMU HALAMGA (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:-

Je, kuna mpango gani wa kutoa Bima za Afya kwa Wafungwa.

WIZARA YA MAJI:

133. MHESHIMIWA DKT. CHARLES STEPHEN KIMEI (VUNJO):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:-

Je, kwa nini Serikali isiingize gharama za mita za maji kwenye vitabu vyao vya fedha badala ya kuweka pale inapounganishwa maji.

WIZARA YA UJENZI NA UCHUKUZI:

134. MHESHIMIWA EDWIN ENOSY SWALLE (LUPEMBE):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi:-

Je, lini ujenzi wa barabara ya Kibena *Stop*, Lupembe hadi Madeke kwa kiwango cha lami utaanza.

**135. MHESHIMIWA DKT. CHRISTINA
CHRISTOPHER MNZAVA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi:-

Je, ni lini Serikali itaanza na kukamilisha ujenzi wa barabara ya Kahama – Solwa hadi Mwanza kwa kiwango cha lami.

IV. HOJA ZA SERIKALI:

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (UTUMISHI NA
UTAWALA BORA):**

Kwamba, Bunge sasa likubali kupokea na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais (Utumishi na Utawala Bora) kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024.

**DODOMA
19 APRILI, 2023**

**N.J. MWIHAMBI, *ndc*
KATIBU WA BUNGE**